TANGAZO LA SERIKALI NA. 597 la tarehe 25/8/2023

# SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,
(SURA YA 414)

# AMRI YA UGATUZI WA MAMLAKA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI YA MWAKA 2023

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 22)*

## MPANGILIO WA AYA

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Maelezo*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

## SEHEMU YA PILI
## UGATUZI WA MAMLAKA

4. Ugatuzi kwa Kamati.
5. Ugatuzi kwa Kamati ya Sheria.
6. Ugatuzi kwa Menejimenti.
7. Ugatuzi kwa Divisheni.
8. Ugatuzi kwa wakaguzi.
9. Kufutwa kwa Amri.

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(SURA YA 414)

______

**AMRI**

_____

AMRI YA UGATUZI WA MAMLAKA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI YA MWAKA 2023
*(Imetolewa chini ya kifungu cha 22)*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Ugatuzi wa Mamlaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya mwaka 2023.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kwa mamlaka yote ambayo Bodi imekasimisha kwa Kamati zake, Menejimenti, Divisheni na waajiriwa wa Mamlaka na itaainisha utekelezaji wa majukumu hayo.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka;

"Divisheni" maana yake ni Divisheni ya Mamlaka inayohusika na usikilizaji wa malalamiko kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya Sita ya Sheria;

"Kamati ya Sheria na Masuala ya Kiutawala" maana yake ni Kamati ya Sheria na Masuala ya Kiutawala ya Bodi;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria;

"Menejimenti" maana yake ni Menejimenti ya Mamlaka;

"mkaguzi" maana yake ni afisa wa Mamlaka anayehusika kusimamia uzingatiaji wa sheria;

Sura ya 414

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

## SEHEMU YA PILI
## UGATUZI WA MADARAKA

Ugatuzi kwa Kamati

4. Bodi inagatua mamlaka yake yaliyoainishwa kwenye Mkataba wa Bodi kwa Kamati ya Nishati, Kamati ya Maji, Kamati ya Ukaguzi na Kinga za Hatari na Kamati ya Sheria naMasuala ya Kiutawala.

Ugatuzi wa mamlaka kwa Kamati ya Sheria na Masuala ya Kiutawala

5. Bodi inagatua kwa Kamati ya Sheria na Masuala ya Kiutawala mamlaka yake ya kujadili na kuamua malalamiko yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sehemu ya Sita ya Sheria.

Ugatuzi wa mamlaka kwa Menejimenti

6. Bodi inagatua kwa Menejimenti mamlaka yake ya-

(a) kutoa amri za utekelezaji kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha Sheria;
(b) kutoa amri ya kufunga miundombinu inayodhibitiwa;
(c) kuchukua hatua zozote za kuadhibu;
(d) kumtaka mtu yeyote kusambaza bidhaa au huduma;
(e) kutoa wito wa kumtaka mtu yeyote kuwasilisha taarifa yoyote, kutoa nyaraka kwa Mamlaka au kufika mbele ya Mamlaka kutoa ushahidi kwa mdomo;
(f) kuamuru utekelezaji wa jambo mahsusi; na
(g) kutoa amri nyingine yoyote kadri itakavyoonekana muhimu.

Ugatuzi kwa Divisheni

7. Bodi inagatua kwa Divisheni mamlaka yake ya kusikiliza na kuamua maombi ya maamuzi madogo na kutoa amri za kuondoa malalamiko kwa malalamiko yaliyoondolewa kwa mujibu wa Sehemu ya Sita ya Sheria.

Ugatuzi kwa wakaguzi

8. Bodi inagatua kwa wakaguzi mamlaka yake ya kusimamia uzingatiaji wa sheria ikijumuisha ufungaji wa miundombinu, jengo au eneo lolote linalodhibitiwa au chombo cha usafirishaji kuhusiana na masuala ya ubora au pale ambapo kuna hatari katika afya, usalama au mazingira.

Kufutwa kwa Amri TS Na. 247 la 2012

9. Amri ya Ugatuzi wa Mamlaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya mwaka, 2012 imefutwa

Dodoma, ..........................., 2023

JAMES. A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*